Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 05 Issue: 01 | November-2026

EAJK

Mchango wa Asasi Mbalimbali Katika Kusuluhisha Mizozo ya Ardhi: Tathmini ya Riwaya ya Kovu Moyoni (Habwe, 2014)

Author
Mary K. Njeru
Author's email: mnjeru@chuka.ac.ke

Chuka University, Kenya.

Cite this article in APA
Njeru, M. K. (2026). Mchango wa asasi mbalimbali katika kusuluhisha mizozo ya ardhi: Tathmini ya riwaya ya *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014). *Eastern Africa journal of Kiswahili, 5*(1), 201–212. https://doi.org/10.51317/ghccds82

OPEN ACCESS
A publication of Editon Consortium Publishing (online)

Article history
Received: 2026-09-04
Accepted: 2026-10-08
Published: 2026-11-16

Scan this QR to read the paper online

Copyright: ©2026 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

Ikisiri

Makala hii ilichunguza namna asasi mbalimbali zinavyoshiriki katika kuzuia, kudhibiti na kusuluhisha mizozo ya ardhi, pamoja na kujenga upya jamii baada ya migogoro, kama inavyowasilishwa katika riwaya ya *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014). Mizozo ya ardhi nchini Kenya ina mizizi ya kihistoria inayohusishwa na unyakuzi wa ardhi wakati wa ukoloni, mifumo ya umiliki isiyo sawa na matumizi ya ardhi katika ushindani wa kisiasa. Kwa kutumia muundo wa kimaelezo na uchanganuzi wa matini, data ilikusanywa kwa kusoma riwaya kwa kina, kutambua na kuteua dondoo zinazohusu asasi mbalimbali na kuzipanga katika mada za serikali na vyombo vya usalama, mahakama, viongozi wa kisiasa, taasisi za kidini, mashirika yasiyo ya serikali, vyombo vya habari, wapatanishi na mchango wa wananchi. Uchanganuzi uliongozwa na Nadharia ya Baadaukoloni ukizingatia mihimili ya urithi wa ukoloni, mamlaka na unyonyaji, pamoja na upinzani na ukombozi. Matokeo yanaonyesha kuwa asasi hizi zina majukumu tofauti: baadhi huzuia au kudhibiti vurugu, nyingine husaidia waathiriwa na nyingine hushiriki katika upatanishi na ujenzi upya wa jamii. Hata hivyo, uzembe, matumizi mabaya ya mamlaka na maslahi ya kisiasa hudhoofisha juhudi hizo. Makala imebainisha kuwa serikali na vyombo vya usalama vinaweza kurejesha usalama, mahakama zinapaswa kuhakikisha haki na mashirika yasiyo ya serikali na taasisi za kidini zinaweza kusaidia waathiriwa. Inapendekeza taasisi za serikali zinazohusika na ardhi ziimarishe uwazi, uwajibikaji na utoaji wa maamuzi kwa wakati kuhusu madai ya umiliki na fidia. Inachangia katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili kwa kuonyesha jinsi riwaya inavyowakilisha kwa pamoja uwezo na mipaka ya asasi katika kushughulikia mizozo ya ardhi.

Maneno muhimu: Ardhi, asasi, Baadaukoloni, fasihi ya Kiswahili, mizozo ya ardhi.

UTANGULIZI

Makala hii iilchunguza namna asasi mbalimbali zinavyoshiriki katika kuzuia, kudhibiti na kusuluhisha mizozo ya ardhi, pamoja na kujenga upya jamii baada ya migogoro, kama inavyowasilishwa katika riwaya ya *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014). Ingawa tafiti zimejadili historia ya umiliki wa ardhi, athari za migogoro, sheria na nafasi ya siasa, bado haijaelezwa vya kutosha jinsi kazi ya kifasihi inavyowakilisha kwa pamoja majukumu tofauti ya asasi katika hatua za kuzuia migogoro, kudhibiti vurugu, kutatua madai ya ardhi na kujenga upya jamii. Kwa hivyo, makala hii inachunguza si tu mchango chanya wa asasi bali pia namna uzembe, matumizi mabaya ya mamlaka na maslahi ya kisiasa yanavyoweza kuzifanya kuwa sehemu ya tatizo.

Riwaya ya *Kovu Moyoni* inafaa kwa uchunguzi huu kwa kuwa matukio yake yanahusisha serikali, polisi na jeshi, mahakama na magereza, viongozi wa kisiasa, taasisi za kidini, mashirika yasiyo ya serikali, vyombo vya habari, wapatanishi na wananchi. Kwa kuchanganua matukio hayo, makala inatofautisha hatua za kurejesha usalama na juhudi za kutatua chanzo cha mgogoro wa ardhi. Hivyo, makala hii inaaangazia jinsi ambavyo riwaya teule inasawiri mchango na udhaifu wa asasi mbalimbali katika kushughulikia mizozo ya ardhi, na hali ya urithi wa ukoloni na mahusiano ya mamlaka.

Ardhi ni rasilimali inayowezesha makazi, kilimo na uzalishaji mali, na pia hujenga utambulisho na urithi wa jamii. Hata hivyo, umuhimu wake huifanya kuwa kitovu cha ushindani pale haki za umiliki, ugawaji na usimamizi zinapokosekana au zinapotumiwa kisiasa (Njeru, 2018). Nchini Kenya, suala hili linaweza kueleweka kwa kuzingatia historia ya unyakuzi wa ardhi na mifumo ya umiliki iliyoanzishwa wakati wa ukoloni. Nyukuri (1997) anaeleza kuwa unyakuzi wa ardhi yenye rutuba uliwanyima Waafrika maeneo yao na kuwaacha baadhi yao katika hali ya kuwa maskwota. Urithi huo wa kihistoria unatoa muktadha wa kuelewa madai ya ardhi na hisia za kutengwa zinazoibuliwa katika jamii za baada ya ukoloni.

Athari za mizozo ya ardhi hujitokeza katika viwango tofauti. Migogoro ya umiliki huhusu madai yanayokinzana kuhusu haki ya kumiliki au kutumia ardhi; migogoro ya kisiasa inayohusishwa na ardhi hutokana na matumizi ya madai hayo katika kugombea mamlaka; nayo migogoro ya kikabila inaweza kutumiwa kuhamasisha uhasama kati ya makundi mbalimbali. Nyiri (2014) anaonyesha athari za mizozo ya kikabila kwa usalama na maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Ni muhimu kutofautisha aina hizi kwa sababu si kila tukio la vurugu ni suluhisho la mgogoro wa umiliki: kurejesha usalama hudhibiti vurugu, lakini haki ya ardhi huhitaji uchunguzi na maamuzi ya haki.

Katika fasihi ya Kiswahili, masuala ya ardhi yanawasilishwa kama sehemu ya mahusiano ya mamlaka, utambulisho na haki. Gonye na wenzake (2020) wanaeleza kuwa fasihi huakisi mazingira ya kijamii na kisiasa ambamo kazi huzalishwa. Masibo (2015) anajadili uwakilishi wa diskosi za ardhi katika kazi za fasihi za Kenya, huku Njeru na wenzake (2022a) wakionyesha uwezo wa fasihi kuibua matatizo ya kimazingira. Tafiti hizi zinaweka msingi wa kuichunguza ardhi kifasihi; hata hivyo, hazijibu moja kwa moja swali la namna asasi tofauti zinavyowakilishwa katika kuzuia, kushughulikia na kurekebisha madhara ya mizozo ya ardhi katika riwaya ya *Kovu Moyoni*.

Katika muktadha huu, makala ilichunguza *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014), riwaya inayowasilisha jamii inayokumbwa na mizozo ya ardhi, uhasama wa kikabila na matumizi ya mamlaka kisiasa. Lengo kuu ni kuchanganua mchango na udhaifu wa asasi zinazohusika katika mchakato wa kushughulikia migogoro hiyo. Uchambuzi unajikita katika namna serikali na vyombo vya usalama vinavyodhibiti vurugu, mahakama zinavyohusishwa na haki, wanasiasa wanavyoathiri migogoro, na namna dini, mashirika yasiyo ya serikali, vyombo vya habari, wapatanishi na wananchi wanavyosaidia katika upatanishi na ujenzi upya wa jamii. Nadharia ya Baadaukoloni inatumika kutafsiri uhusiano kati ya urithi wa ukoloni, mamlaka na upinzani.

MAPITIO YA MAANDISHI

Ardhi na Mizozo ya Ardhi Nchini Kenya

Ardhi ni msingi wa shughuli nyingi za kijamii na kiuchumi. Njeru na wenzake (2022b) wanaonyesha umuhimu wa mazingira na rasilimali zake katika maisha ya jamii. Ardhi, kama sehemu muhimu ya mazingira, huwezesha uzalishaji wa chakula, makazi na shughuli nyingine za kiuchumi. Aidha, kwa jamii nyingi, ardhi huhusishwa na utambulisho na urithi wa kitamaduni ikiwemo umiliki wa ardhi.

Gatimu (2014) anaeleza kwamba suala la ardhi nchini Kenya limekuwa nyeti tangu kipindi cha ukoloni.

Nyukuri (1997) anaonyesha kuwa unyakuzi wa ardhi uliofanywa na wakoloni uliwanyima Waafrika maeneo yao na kuwafanya baadhi yao kuwa maskwota. Hali hii ilichangia kuibuka kwa upinzani dhidi ya utawala wa kikoloni. Klopp na Lumumba (2017) nao wanaonyesha kuwa mizozo ya ardhi nchini Kenya ina uhusiano na historia ya sera za kikoloni kuhusu umiliki na usimamizi wa ardhi.

Njogu (2015) anaonyesha uhusiano uliopo baina ya ardhi na siasa nchini Kenya. Ardhi imekuwa ikitumika katika mijadala ya uchaguzi na uhamasishaji wa makundi ya kijamii. Kwa hivyo, mizozo ya ardhi haiwezi kutenganishwa na masuala ya mamlaka na siasa.

Masibo (2015) anachunguza diskosi za ardhi katika kazi za fasihi za Kenya na hivyo kuonyesha namna ardhi inavyoweza kuwasilishwa kama suala la mamlaka na ukosefu wa usawa. Utafiti huo unaweka msingi wa usomaji wa kifasihi wa suala la ardhi, lakini lengo lake si kuchanganua kwa kina majukumu ya asasi katika hatua mbalimbali za kushughulikia migogoro. Makala hii inapanua mjadala huo kwa kuelekeza uchunguzi katika *Kovu Moyoni* na katika uhusiano kati ya asasi, utatuzi wa mizozo ya ardhi na urithi wa ukoloni.

Athari za Mizozo ya Ardhi

Nyiri (2014) anaonyesha kwamba mizozo ya kikabila inaweza kuathiri uchumi, usalama na maendeleo ya jamii. Mizozo husababisha vifo, uharibifu wa mali, kuhama kwa watu na kuvurugika kwa shughuli za kiuchumi. Aidha, elimu huathirika kwa sababu shule zinaweza kufungwa au wanafunzi kulazimika kuhama maeneo yao.

Kwa mujibu wa Omboi na Gachaba (2014), matatizo ya umiliki wa ardhi yanaweza kuchangia kuibuka kwa tatizo la maskwota. Pia, uuzaji wa mashamba ya familia bila mashauriano ya kutosha unaweza kuzua migogoro na kupoteza haki za baadhi ya wanajamii.

Matokeo ya utafiti wa Njoroge (2013) yanathibitisha kuwa udhaifu wa sheria na taasisi zinazoshughulikia masuala ya ardhi unaweza kuyafanya matatizo yaendelee. Hoja hii ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu *Kovu Moyoni* inaonyesha baadhi ya wananchi wakitafuta haki kupitia taasisi mbalimbali bila kupata msaada unaotarajiwa.

Makunike (2014) anaonyesha uhusiano baina ya umiliki wa ardhi na umaskini nchini Zimbabwe. Historia ya ubaguzi wa kikoloni katika umiliki wa ardhi iliendelea kuathiri hali ya kiuchumi ya watu katika kipindi cha baada ya ukoloni. Hoja hii inahusiana na Kenya kwa sababu matatizo ya sasa ya ardhi yanaweza kueleweka kwa kurejelea historia ya mifumo ya kikoloni.

Fasihi na Uwakilishi wa Masuala ya Jamii

Kwa mujibu wa Gonye na wenzake (2020), fasihi ni zao la kipindi ambamo imeibuka na huweza kuwakilisha matukio, matatizo na mafanikio ya jamii. Kwa hiyo, kazi ya fasihi inaweza kuwa chanzo muhimu cha kuelewa masuala ya kijamii.

Opondo na wenzake (2025) wanaeleza kuwa fasihi ni kielelezo cha hali halisi ya jamii na kwamba msanii ni sehemu ya jamii anayoieleza. Kwa mtazamo huu, *Kovu Moyoni* inaweza kuchukuliwa kuwa kazi inayotoa tafakuri kuhusu matatizo ya jamii ya Kenya, hususan mizozo ya ardhi, ukabila, siasa na matumizi ya mamlaka.

Njeru na wenzake (2022b) katika utafiti wao kuhusu motifu za kimazingira wanaonyesha kwamba fasihi inaweza kutumika kuangazia matatizo yanayoikumba jamii. Utafiti wao kuhusu riwaya ya *Majira ya Utasa* (Arege, 2015) unaonyesha kuwa masuala ya mazingira yanaweza kuwasilishwa kifasihi ili kuonyesha chanzo, athari na uwezekano wa kuyatatua. Ingawa utafiti wao haukulenga mizozo ya ardhi, una umuhimu katika utafiti huu kwa sababu ardhi ni sehemu muhimu ya mazingira na rasilimali zinazotegemewa na jamii.

Asasi na Utatuzi wa Mizozo ya Ardhi

Njoroge (2013) na Maina (2015) wanaonyesha umuhimu wa taasisi za kisheria katika kushughulikia migogoro ya ardhi. Hata hivyo, ufanisi wa taasisi hizo hutegemea utekelezaji wa sheria, uwezo wa taasisi na upatikanaji wa haki. Kwa mujibu wa Nyiri (2014), mashirika yasiyo ya serikali na taasisi za kidini yalichangia kuwasaidia waathiriwa wa migogoro kurejea katika maeneo yao na kupata huduma muhimu. Jambo hili linaonyesha kuwa serikali si mhusika pekee katika mchakato wa kutatua migogoro.

Aidha, Njogu (2015) anaonyesha uhusiano kati ya uchaguzi, siasa na ardhi nchini Kenya. Matokeo ya utafiti yake inasaidia kuelewa kuwa wanasiasa wanaweza kuathiri umiliki, ugawaji na usimamizi wa ardhi kwa kutumia madai ya kihistoria au utambulisho wa makundi katika kujenga uungwaji mkono. Katika *Kovu Moyoni*, mhusika Mwamba anahusishwa na mashambulizi na uhamasishaji wa vijana. Usawiri huu unaonyesha upande wa kichochezi wa uongozi wa kisiasa; haupaswi kuchanganywa na jukumu la uongozi unaowajibika katika kutafuta suluhisho.

Nadharia ya Baadaukoloni

Nadharia ya Baadaukoloni inahusishwa na mjadala kuhusu athari za ukoloni katika jamii zilizotawaliwa na namna athari hizo zinavyoendelea baada ya uhuru. Childs na Williams (1997) wanaeleza kuwa ukoloni uliathiri jamii za Kiafrika kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Naye Fanon (1961) anaonyesha kwamba kuondoka kwa mkoloni hakumaanishi kwamba mifumo yote ya ukoloni hasa iliyohusishwa na umiliki wa ardhi iliondoka.

Katika muktadha wa ardhi nchini Kenya, nadharia hii ni muhimu kwa sababu mifumo ya umiliki wa ardhi iliyowekwa wakati wa ukoloni iliendelea kuwa na athari katika kipindi cha baada ya uhuru. Ndiposa Masibo (2015) anaonyesha umuhimu wa kuangalia suala la ardhi kwa kuzingatia historia ya ukoloni na mifumo ya mamlaka iliyorithiwa.

Nadharia hii inadhihirika katika *Kovu Moyoni* kupitia masuala ya unyakuzi wa ardhi, tofauti za kitabaka, ukabila, siasa, matumizi ya mamlaka na mapambano ya wananchi kutafuta haki. Pia inasaidia kuelewa kwa nini baadhi ya viongozi wa baada ya uhuru wanaweza kuendeleza mifumo ya unyonyaji ambayo ina mizizi katika utawala wa kikoloni.

Pengo la Utafiti

Kuna tafiti na maandishi mbalimbali kuhusu ardhi au migogoro inayohusiana na ardhi nchini Kenya. Tafiti kama Nyukuri (1997), Nyiri (2014), Njoroge (2013), Maina (2015), Njogu (2015) na Masibo (2015) zimejadili vipengele vya kihistoria, kijamii, kisheria, kisiasa na kifasihi vya suala hili. Hata hivyo, katika maandishi yaliyopitiwa, haijachanganuliwa kwa pamoja namna riwaya moja ya Kiswahili inavyowakilisha asasi zinazohusika katika kuzuia migogoro, kudhibiti vurugu, kushughulikia haki na kujenga upya jamii, huku ikitathmini pia udhaifu wao kwa kutumia mtazamo wa Baadaukoloni. Hili ndilo pengo mahususi ambalo makala hii inalenga kulijaza.

Kwa kulijaza pengo hilo, Makala hii ilichanganua makundi ya asasi katika *Kovu Moyoni* na kutathmini mchango na mipaka ya kila kundi. Uchanganuzi unatofautisha hatua za kabla ya mgogoro, wakati wa vurugu na baada ya mgogoro, badala ya kuzichukulia hatua zote kama utatuzi mmoja.

Kiunzi cha Nadharia

Nadharia ya Baadaukoloni huchunguza namna ukoloni ulivyounda mifumo ya mamlaka, uchumi, utambulisho na uwakilishi, pamoja na namna mifumo hiyo inavyoendelea au kupingwa baada ya uhuru. Childs na Williams (1997) wanaeleza kuwa baadaukoloni si kipindi kinachofuata tu ukoloni, bali pia ni mkabala wa kuchunguza athari na urithi wa ukoloni katika jamii na utamaduni. Vile vile, Fanon (1961) anaonya kuwa uhuru wa kisiasa hauhakikishi kuondoka kwa miundo ya unyonyaji, kwani tabaka la wenye mamlaka wa ndani linaweza kurithi na kuendeleza mifumo iliyowekwa na wakoloni. Kwa hiyo, nadharia hii inafaa kuchunguza ardhi kama rasilimali inayohusishwa na historia ya unyakuzi, mamlaka na utambulisho.

Katika makala hii, mtazamo wa Fanon (1961) kuhusu mwendelezo wa miundo ya kikoloni na mjadala wa Childs na Williams (1997) kuhusu athari za ukoloni ndio msingi wa kutafsiri matukio. Nadharia inatumiwa kama lenzi ya uchanganuzi, si kama dai kwamba kila tukio katika riwaya limetokana moja kwa moja na ukoloni.

Uchanganuzi umezingatia mihimili mitatu inayotokana na mjadala wa baadaukoloni. Mhimili wa urithi wa ukoloni unachunguza jinsi mifumo ya umiliki na ugawaji wa ardhi iliyoanzishwa wakati wa ukoloni inavyoendelea kuathiri madai ya ardhi na nafasi za wananchi baada ya uhuru. Mhimili wa mamlaka na unyonyaji unachunguza namna viongozi au taasisi zenye nguvu zinavyotumia mamlaka, sheria na rasilimali kwa manufaa binafsi au ya tabaka fulani. Mhimili wa upinzani na ukombozi unachunguza hatua za wananchi na makundi mengine kupinga ukandamizaji, kudai haki, kujenga mshikamano na kuunda mahusiano mapya yasiyotawaliwa na chuki za kikabila.

Katika uchanganuzi, urithi wa ukoloni unahusishwa hasa na historia ya madai ya ardhi na kushindwa kwa wananchi kupata fidia au haki; mamlaka na unyonyaji vinatumika kuchunguza urasimu, matumizi mabaya ya polisi na uchochezi wa wanasiasa; upinzani na ukombozi vinatumika kutafsiri upatanishi, mshikamano wa wananchi na juhudi za kujenga upya maisha. Nadharia hii imechaguliwa kwa sababu inaunganisha historia ya ardhi na mahusiano ya mamlaka. Hata hivyo, matukio yanafafanuliwa pia kwa kuzingatia muktadha wake wa kijamii na ushahidi wa riwaya.

MBINU ZA UTAFITI

Utafiti ulitumia muundo wa kimaelezo wa uchanganuzi wa matini na ulifanywa maktabani. *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014) iliteuliwa kimakusudi kwa sababu inawasilisha mizozo ya ardhi pamoja na wahusika na asasi zinazohusika katika kudhibiti vurugu, kutafuta haki na kujenga upya jamii. Data ilikusanywa kwa kusoma riwaya nzima kwa kina na kurejelea tena sehemu zilizohusiana na lengo la utafiti. Dondoo zilitambuliwa kwa kutumia vigezo vitatu: kutajwa kwa asasi au mwakilishi wake; kuhusika kwa tukio katika kuzuia, kuchochea, kudhibiti au kutatua mzozo; na kuonyesha athari kwa haki ya ardhi, usalama, maridhiano au maisha ya waathiriwa.

Dondoo zilirekodiwa pamoja na nambari za kurasa na kupangwa katika makundi ya mada yaliyolingana na asasi husika. Uchanganuzi ulifanyika kwa kutafsiri muktadha wa kila dondoo, kubainisha mchango au udhaifu wa asasi, kisha kuhusisha tafsiri hiyo na mhimili unaofaa wa nadharia ya Baadaukoloni. Uaminifu uliimarishwa kwa kurejea dondoo katika muktadha wa riwaya nzima, kuhifadhi maneno na nambari za kurasa kama zilivyo katika toleo lililotumika, na kulinganisha mifano zaidi ya mmoja pale ilipowezekana. Utafiti huu unahusu matini moja; kwa hiyo, matokeo yake hayakusudiwi kuwakilisha riwaya zote za Kiswahili.

MATOKEO YA UTAFITI

Mchango wa Serikali katika Kusuluhisha Mizozo ya Ardhi

Kupitia *Kovu Moyoni*, Habwe anaonyesha kuwa serikali ina jukumu kubwa katika kurejesha amani na usalama wakati wa mizozo ya ardhi. Jeshi la taifa linapotumwa katika maeneo yaliyokumbwa na mashambulizi, shughuli za kawaida huanza kurejea:

> "…Jeshi la taifa lilipotia guu lake Rama uhai ulirudi. Wafanyabiashara walianza kurudi masokoni. Watu waliokuwa kwa jamaa zao wakarudi nyumbani. Msimu wa upanzi uliokuwa umechelewa ulipigwa jeki. Matrekta yalilima katika mashamba. Nayo kelele ya watu wa kuswaga ng'ombe wa kulima ikasikika katika baadhi ya mashamba…" (Habwe, 2014, uk. 118).

Dondoo hili linaonyesha kuwa serikali kupitia jeshi ina uwezo wa kurejesha hali ya usalama inayowezesha wananchi kurudi katika makazi yao na kuendelea na shughuli za kiuchumi. Kurudi kwa wafanyabiashara masokoni na wakulima mashambani kunaonyesha uhusiano baina ya usalama na matumizi ya ardhi. Bila amani, ardhi haiwezi kutumiwa kwa tija.

Hata hivyo, Habwe haishii kuonyesha serikali kama chombo cha suluhisho. Anaonyesha pia umuhimu wa serikali kuwakamata na kuwafikisha mbele ya sheria watu wanaochochea mizozo:

> "… kulikuwa na fununu kwamba Jeshi la Taifa lilimtafuta ili kumtia nguvuni na kumfungulia mashtaka. Mawakala wake kama vile Mustafa walikuwa wametiwa nguvuni wakingojea siku za kesi zao kufanywa…familia ya Mwamba ilishikwa na wasiwasi iliposikia anatafutwa na polisi kutiwa nguvuni kwa ajili ya maasi ya Rama…" (Habwe, 2014, uk. 137).

Mwamba ni mwanasiasa mwenye ushawishi ambaye anahusishwa na kuendesha kundi la Jeshi la Vijana. Kwa hiyo, hatua ya kumtafuta na kumtia mbaroni inaonyesha kwamba serikali inaweza kutumia vyombo vyake kukomesha uhalifu na kuwawajibisha wachochezi.

Hata hivyo, kwa mtazamo wa Baadaukoloni, Fanon (1961) anasisitiza kuwa uhuru wa kisiasa hauondoi moja kwa moja mifumo ya ukandamizaji. Serikali ya baada ya ukoloni inaweza kurithi na kuendeleza mifumo ya utawala inayowanyima wananchi haki na uhuru. Kwa hivyo, nafasi ya serikali katika kusuluhisha mizozo ya ardhi inaweza kutazamwa kwa jicho la

tahadhari. Hii ni kwa sababu serikali inaweza kuwa chombo cha kulinda wananchi au chombo cha kuendeleza ukandamizaji. Habwe anaonyesha pande zote mbili. Serikali inapotenda kwa haki hurejesha amani, lakini inaposhindwa kuwajibika huwa sehemu ya tatizo.

Udhaifu wa Taasisi za Serikali

Pamoja na kuonyesha mchango wa serikali, Habwe anakosoa udhaifu wa taasisi zinazohusika na masuala ya ardhi. Mama yake Meja-K anatafuta fidia bila mafanikio:

> "… hapo ndipo akili zake zilipoanza kurudia kwenye ile sehemu ya baba yake ya shamba la bwanyenye. Walikuwa wameambiwa wangefidiwa pesa Fulani. Mama yake alidai hizo pesa miaka na mikaka bila mafanikio. Mama yake Meja-K, Bi. Kimaka, alikwenda kwa Chifu Ngata miaka nenda miaka rudi. Baadaye kwa afisa wa wilaya. Hatimaye katika halmashauri za mashamba. Hapana aliyeelewa jambo alilokuwa akilisema. Wahusika aliowafuata walijifanya kutoelewa kile ambacho alikuwa anakisema." (Habwe, 2014, uk. 17).

Dondoo hili linaonyesha namna taasisi zinavyoweza kumwangusha mwananchi anayetarajia haki. Bi. Kimaka anapita katika ngazi mbalimbali za utawala lakini hapati suluhisho. Hali hii inaonyesha tatizo la urasimu na ukosefu wa uwajibikaji.

Mfano mwingine unatolewa kupitia babake Meja-K:

> "Meja-K alikumbuka juhudi za babake za kusalimisha Shamba lake. Baba mzazi alipanda vilima akashuka mabondeni. Aliingia kila korti. Alibisha kila mlango husika wa serikali lakini hakufaulu kulisalimisha shamba lake. Kishamba kilichobaki hakikuweza kuhimili familia yao ya watoto saba." (Habwe, 2014, uk 16).

Dondoo hili linaonyesha kuwa tatizo la ardhi linaweza kudumu kwa muda mrefu iwapo taasisi zinazopaswa kutoa haki hazitekelezi wajibu wao. Mtazamo wa Baadaukoloni huangazia namna mifumo ya mamlaka katika jamii za baada ya ukoloni inavyoendeleza mahusiano ya utawala, udhibiti na unyenyekevu wa wananchi. (Mbembe, 1992). Aidha, Fanon (1961) anaeleza kuwa viongozi wa baada ya ukoloni wanaweza kuendeleza mifumo ya ukandamizaji iliyorithiwa kutoka katika utawala wa kikoloni. Hali hii inaweza kufasiriwa kama mwendelezo wa mifumo ya mamlaka inayomweka mwananchi wa kawaida katika nafasi ya chini na yenye uwezo mdogo wa kupata haki.

Nafasi ya Dini

Dini inasawiriwa kama chombo cha maadili na upatanisho. Katika mazishi ya Chifu Ngata, padre anatumia nafasi yake kuonya jamii:

> "Chifu Ngata alizikwa baada ya siku mbili. Mazishi yake yalikuwa kama ya mtoto mchanga. Ni watu wachache waliojisabilia nyoyo zao na kuhudhuria mazishi hayo. Watu waliogopa kusema lolote baada ya kuonywa vikali na Jeshi la Vijana. Hata mahubiri yaliyotolewa siku hiyo yalikuwa mafupi. Padre aliwaonya wanadamu na kuwatahadharisha na matukio ya siku za mwisho." (Habwe, 2014, uk 49).

Padre anatumia mahubiri kuwakumbusha wanajamii kuhusu utu na madhara ya matendo ya kikatili. Kwa hiyo, dini inaweza kuwa chombo cha kuhimiza maadili yanayosaidia kuzuia migogoro. Hata hivyo, Habwe anaonyesha kwamba katika mazingira ya hofu, hata viongozi wa dini wanaweza kushindwa kutoa ujumbe kwa uhuru. Mahubiri yanakuwa mafupi kutokana na hali ya vitisho. Hii inaonyesha namna migogoro inavyoweza kudhoofisha hata asasi ambazo kwa kawaida zinatarajiwa kuwa nguzo za maadili.

Hali hii inaweza kufasiriwa kwa mtazamo wa Baadaukoloni kwa mujibu wa Fanon (1961), anayeonyesha namna mifumo ya mamlaka na ukandamizaji inavyoweza kuathiri uhuru wa wananchi katika jamii za baada ya ukoloni. Kwa msingi huo, hali ya Padre kushindwa kutoa mahubiri kwa uhuru inaweza kuchukuliwa kama kielelezo cha namna mazingira ya ukandamizaji yanavyoweza kudhoofisha

uhuru wa taasisi za dini katika kutekeleza wajibu wake wa kijamii na kimaadili.

Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Serikali

Mashirika yasiyo ya serikali yana nafasi muhimu katika kuwasaidia waathiriwa wa migogoro. Hali hii inaonekana kupitia Shirika la `Chunga Ndugu Yako`:

> "Mungu ni mkubwa," Boke alisema kwa dhati akizuia machozi, "kama si Mungu hatungekuwa hai. Tumeishi na simba katika pango lake lakini bado tuko hai," Nifreda alisema. Ile hasira yake ilikuwa imeshuka. Aliajiriwa kazi na Shirika la Chunga Ndugu Yako linalowasaidia watu kurudi nyumbani. Shirika hili limemsaidia kuyaendeleza na kuyamaliza tena masomo yake katika Chuo Kikuu cha Tandika. "Nikusaidie vipi, mama," Nifreda alimuuliza Boke. Alipomkagua tena akashangaa. Boke alikuwa mwanamke mnene, mwekundu lakini leo amekonda kama ufito wa mwanzi." (Habwe, 2014, uk. 98).

Dondoo hili linaonyesha kuwa mashirika yasiyo ya serikali yanaweza kutoa msaada wa kibinadamu, kuwawezesha waathiriwa kurejea makwao na kusaidia vijana kuendelea na masomo. Nifreda, ambaye ni mwathiriwa wa mzozo, anapata fursa ya kujenga upya maisha yake.

Hoja hii inalingana na maoni ya Nyiri (2014), anayeeleza kuwa mashirika yasiyo ya serikali na taasisi za kidini yalikuwa na mchango katika kuwasaidia waathiriwa wa migogoro ya Mlima Elgon kurejea katika maeneo yao na kupata huduma muhimu. Kwa hivyo, fasihi inathibitisha kwa njia ya kifani umuhimu wa asasi zisizo za serikali katika kujenga upya maisha baada ya migogoro.

Nafasi ya Viongozi wa Kisiasa

Jambo linalodhihirika kupitia uchanganuzi wa *Kovu Moyoni* ni mchango hasi wa wanasiasa pale wanapotumia migogoro ya ardhi kwa manufaa yao, wala si nafasi ya uongozi wa kisiasa katika kutatua migogoro hiyo. Habwe anamhusisha Mwamba na mashambulizi ya Rama:

> "…….Upepo wa mashambulizi ulipovuma, jina moja lilitajwa. Jina la kweli la mwanasiasa huyo aliyelaumiwa na nafsi za wakimbizi ni Tanga, lakini alijulikana sana kwa jina la lakabu, Mwamba…baadhi ya wafuasi wake walimnasibisha na Tom Kisale aliyekuwa mtetezi wa haki za wafanyakazi nchini Tandika. Kwa siku kadhaa Mwamba alipambana na Ngozi ambaye minong'ono ilisema ni mzaliwa kamili wa Lumbasa…" (Habwe, 2014, uk. 52).

Dondoo hili linamwasilisha mwanasiasa anayetajwa kuhusishwa na mashambulizi. Kwa hiyo, mchango wake ni wa kuchochea na kukuza mgogoro badala ya kuutatua. Siasa huathiri ardhi pale madai ya umiliki na tofauti za kijamii zinapotumiwa kuhamasisha wafuasi, kuhalalisha ubaguzi au kuimarisha mamlaka. Kwa mtazamo wa Baadaukoloni, matumizi hayo ya mamlaka yanaendeleza mfumo ambapo wenye nguvu hunufaika huku wananchi wa kawaida wakibeba gharama za vurugu. (Mamdani, 1996). Hivyo, matumizi ya mamlaka kwa manufaa ya mtu binafsi yanaweza kufasiriwa kama mwendelezo wa mfumo wa utawala unaowatenga wananchi wa kawaida na kuwapa wenye nguvu fursa ya kunufaika na rasilimali za jamii. Kwa hivyo, utafiti huu unathibitisha kuwa uwajibikaji wa viongozi ni kipengele muhimu katika utatuzi wa mizozo ya ardhi.

Juhudi za Wananchi katika Kusuluhisha Mizozo

Wananchi wenyewe wanaonyeshwa kuwa sehemu muhimu ya suluhisho. Mfano wa wahusika Eddah na Mulota unaonyesha namna mahusiano baina ya watu wa makundi tofauti yanavyoweza kupunguza uhasama:

> "Wageni walikaribishwa nyumbani. Mazungumzo ya ukweli yakaanza. Boke hakuamini yule mpenzi wa mwanawe ndiye aliyetajwa katika mashambulizi mengi pale Siloko. Lakini akakubali ya jana yamepita. Alishughulikia ya leo. Mambo mengi aliamua kumwachia Mungu. Wageni walitumbuizwa. Wakafanya yote kwa utaratibu na hivyo wakawafungulia

> njia mwafaka Eddah na Mulota kuoana." (Habwe, 2014, uk. 114).

Kupitia dondoo hili, Habwe anaonyesha mazungumzo na msamaha kama njia ya kuondoa uhasama. Ndoa ya Eddah na Mulota inakuwa ishara ya kuvuka mipaka ya kikabila na kuimarisha uhusiano wa jamii.

Kwa mtazamo wa Baadaukoloni, hatua hii inaweza kutazamwa kama upinzani dhidi ya fikra zinazowagawa wananchi kwa misingi ya kikabila. Wananchi wanapokataa kurithi chuki na tofauti zilizotumiwa na wenye mamlaka, wanakuwa washiriki katika mchakato wa ukombozi wa kijamii. Kama anavyoeleza Fanon (1961), mifumo ya kikoloni ilitumia migawanyiko ya kikabila na kikanda kudhoofisha umoja wa wananchi. Hivyo, hatua ya wananchi kukataa chuki za kikabila inaweza kufasiriwa kama jitihada za kuvunja urithi wa migawanyiko ya kikoloni na kujenga mshikamano wa kijamii unaowezesha ukombozi wa jamii.

Korti na Magereza

Mahakama ni taasisi muhimu katika kuhakikisha haki inatendeka. Hata hivyo, riwaya ya *Kovu Moyoni* inaonyesha madhara yanayoweza kutokea iwapo uchunguzi hautafanyika ipasavyo. Mwita ananyongwa kwa kosa ambalo hakulitenda:

> "King'ora kililia mara tatu ishara ya kwamba Mwita alikuwa amenyongwa tayari. Mama yake alipewa nguo zake akaondoka katika gereza la Raka… Boke alichukia serikali. Alichukia polisi. Alichukia oparesheni nzima hiyo, akachukia wanasiasa waliotia cheche za moto zilizolipua moto uliowaka Rama. Wanasiasa ndio waliotia chombo cha mashambulizi pondo hadi kikaingia baharini." (Habwe, 2014, uk. 132).

Tukio hili linaonyesha udhaifu wa mfumo wa haki. Mtu asiye na hatia anapoteza maisha kutokana na utambulisho usio sahihi. Kwa hiyo, mahakama na vyombo vya usalama vinaposhindwa kufanya uchunguzi wa kina vinaweza kuongeza madhara badala ya kutatua tatizo. Maina (2015) anaeleza umuhimu wa taasisi za kisheria katika utatuzi wa migogoro ya ardhi. Hata hivyo, *Kovu Moyoni* inasisitiza kwamba uwepo wa taasisi hautoshi; taasisi hizo lazima ziwe na uwezo wa kutenda haki bila upendeleo na kwa uwajibikaji.

Nafasi ya Polisi na Askari

Polisi na jeshi wana jukumu la kulinda wananchi na kurejesha usalama. Inspekta Suko anawakilisha askari mwadilifu:

> "Boke alimwazia Inspekta Suko aliyesimama kidete kupinga visa vya Jeshi la vijana. Ilibidi kutoroka kambini kwa kuchelea usalama wake. Ameandikiwa barua ya kumwonya na wanayusi waliokuwa katika Jeshi la Vijana. Suko alikuwa ni polisi aliyekuwa na moyo adimu… hakuwa na kinyongo. Alifahamu kazi yake ya uaskari. Kabla ya msimu wa mashambulizi alijulikana katika kambi ya Lumbasa. Aliamka asubuhi na kukimbia kwa minajili ya mazoezi…" (Habwe, 2014, uk. 13).

Suko anawakilisha askari anayetekeleza wajibu wake bila kuogopa vitisho. Kupitia mhusika huyu, Habwe anaonyesha kwamba askari wanaweza kuwa walinzi wa haki na amani. Hata hivyo, riwaya pia inasawiri askari wanaotumia mamlaka vibaya.

> "…'sema lililokuleta,' polisi alimwambia Boke. 'Nilinajisiwa na polisi,' Boke alisema. 'Polisi yupi?' mkuu wa kituo alimuuliza… Boke alipigwa na butwaa kuona yule polisi aliyemnajisi ndiye yule yule pale kituoni anayefanya kazi… Boke aliganda pale kitini kama jiwe. Alikumbuka usiku ule yule mwanamume aliyefaa kumlinda na madaraka yake yote yale alivyomnajisi na hata kumsababishia kuvuja damu…" (Habwe, 2014, uk. 146).

Dondoo hili linaangazia hali ambapo Boke anapokwenda kuripoti ubakaji, anakutana na askari aliyemdhulumu. Kwa mtazamo wa Baadaukoloni, hali hii inaangaziwa na Fanon (1961) anapoeleza namna

vyombo vya dola katika jamii za baada ya ukoloni vinavyoweza kuendeleza mifumo ya ukandamizaji iliyorithiwa kutoka katika utawala wa kikoloni. Aidha, Mbembe (2001) anafafanua namna mamlaka yanavyoweza kutumiwa kudhibiti na kunyanyasa wananchi.

Kwa msingi huo, kitendo cha polisi kumdhulumu Boke kinaweza kufasiriwa kama matumizi mabaya ya mamlaka ya dola yanayokiuka haki, utu na usalama wa mwananchi. Hivyo, kupitia wahusika Suko na polisi aliyemdhulumu Boke, Habwe anadhihirisha kuwa ufanisi wa taasisi za usalama unategemea matumizi sahihi ya mamlaka, uwajibikaji na ulinzi wa haki za wananchi.

Vyombo vya Habari

Vyombo vya habari vina nafasi ya kuelimisha na kuarifu wananchi kuhusu migogoro. Meja-K anasoma gazeti na kupata habari kuhusu mzozo wa kisiasa:

> "Meja-K alikaa katika kiti cha plastiki akisoma gazeti la siku, The Daily Telegraph. Alirauka leo asubuhi ili kupokea msaada ulioletwa kwa ndege ya helikopta kutoka kwa wahisani na wafadhili …alipata kusoma kuhusu zogo la kitaifa lililofuatia kuhusu viongozi kugombania kura. Lo! Kilikuwa kivumbi kweli. Fahali hao wawili walipopigana nyasi ndizo zilizoumia. Watu waliuana. Watu walilaumiana." (Habwe, 2014, uk. 24).

Dondoo hili linaonyesha kuwa vyombo vya habari vinaweza kutoa taarifa kuhusu migogoro na kuwafanya wananchi kuelewa kinachoendelea. Hata hivyo, Habwe anakosoa hali ambapo habari kuhusu mzozo zinafichwa:

> "… kila siku akawa anatazamia kusafiri lakini kila kulipokucha alikuwa akisikia kadhia za watu kuuawa na hata kunajisiwa. Siku zote alitegea taarifa ya habari lakini hakusikia matangazo yoyote kuhusu mashambulizi ya Rama. Eneo hili likawa ni kama eneo lililo ughaibuni lisilo katika nchi ya Tandika…" (Habwe, 2014, uk. 79–80).

Vyombo vya habari vinaponyamaza, wananchi wananyimwa taarifa muhimu kuhusu usalama wao. Kwa mtazamo wa Baadaukoloni, hali hii inaweza kufasiriwa kwa kutumia mawazo ya Said (1978) anayeonyesha uhusiano uliopo kati ya maarifa, uwakilishi na mamlaka. Aidha, Spivak (1988) katika makala yake anajadili namna makundi yaliyotengwa yanavyoweza kunyimwa nafasi ya kutoa sauti na kusikilizwa.

Kwa msingi huo, kutotolewa kwa taarifa kuhusu mashambulizi ya Rama kunaweza kufasiriwa kama hali inayowafanya wananchi waathiriwa kukosa nafasi ya kusikika na kutambuliwa katika jamii. Hivyo, Habwe anaonyesha umuhimu wa vyombo vya habari katika kusambaza taarifa, kuibua mateso ya wananchi na kutoa nafasi kwa sauti za watu wanaoathiriwa na migogoro.

Nafasi ya Wapatanishi

Wapatanishi wanaweza kusaidia pande zinazopingana kufikia mwafaka. Habwe anaonyesha umuhimu wao kupitia washauri wa kimataifa:

> "Meja-K alisoma kuhusu washauri wa kimataifa waliokuja kuwasuluhisha viongozi hawa wawili waliokuwa mithili ya majogoo kizimbani. Kila mmoja akidai ndiye mshindi. Yule msichana waliyegombania walipewa watu wawili kummiliki na kumdhibiti. Mwafaka huo ukawafanya hao ndugu na marafiki wa muda mrefu watupilie mbali silaha wakaanza mashauriano…" (Habwe, 2014, uk. 24).

Dondoo hili linaonyesha kwamba mazungumzo na upatanishi vinaweza kuondoa uhasama na kuleta mwafaka. Kwa hivyo, wapatanishi wanaweza kuwa muhimu hasa pale ambapo pande zinazogombana haziwezi kufikia suluhisho peke yao. Aidha, upatanishi unaweza kufanywa na wanajamii wenyewe. Hii inaonyesha kuwa suluhisho la mizozo halihitaji kila wakati kuletwa na watu kutoka nje. Jamii inaweza kutumia wazee, viongozi wa dini, familia na makundi mengine kuanzisha mazungumzo. Kwa mtazamo wa nadharia ya Baadaukoloni, Fanon (1961) anasisitiza umuhimu wa wananchi kushiriki kikamilifu katika

mchakato wa ukombozi na kujenga upya jamii zao. Vilevile, Ngũgĩ Wa Thiong'o (1986) anasisitiza umuhimu wa kuthamini maarifa na tamaduni za wenyeji.

Kwa msingi huo, matumizi ya wazee, viongozi wa dini na familia katika upatanishi yanaweza kufasiriwa kama jitihada za jamii kutumia rasilimali na maarifa yake yenyewe katika kutatua migogoro na kujenga amani endelevu. Hivyo, Habwe anadhihirisha umuhimu wa ushiriki wa wananchi katika kutafuta suluhisho la migogoro inayowakabili.

Mielekeo Chanya ya Wananchi

Habwe anaonyesha kwamba amani ya kudumu haiwezi kuletwa na serikali pekee. Wananchi wenyewe lazima washiriki katika kuijenga:

> "…usalama gani? Mbona vinywa vya watu bado vinalalamika? Ubakaji bado ungaliko. Unyang'anyi ungaliko. Rushwa ingaliko na imeshamiri. Wakati ndio utakaoamua hali yetu,"… lazima tulete usalama sisi wenyewe. Mtu wa nje hataweza kuleta usalama. Hajui mkosaji. Sisi ndio tunaojua…" (Habwe, 2014, uk. 133).

Kauli hii inaonyesha kuwa usalama ni jukumu la pamoja. Serikali inaweza kutuma jeshi na polisi, lakini wananchi ndio wanaofahamu mazingira yao na watu wanaoweza kuchochea migogoro. Kwa mtazamo wa Baadaukoloni, mabadiliko ya fikra ni sehemu muhimu ya ukombozi. Wananchi wanapokataa ukabila, chuki na matumizi ya vurugu, wanapinga mifumo ya mawazo inayoweza kutumiwa na wenye mamlaka kuwagawa. Hoja hii inaungwa mkono na Ngũgĩ Wa Thiong'o (1986) anayesisitiza umuhimu wa ukombozi wa kifikra katika kujenga utambulisho na mtazamo huru wa jamii. Kwa msingi huo, ushiriki wa wananchi katika kulinda usalama na kukataa migawanyiko ya kikabila unaweza kufasiriwa kama sehemu ya mchakato wa ukombozi wa kijamii na kujenga mshikamano wa kitaifa.

Majadiliano ya Jumla

Kwa ujumla, matokeo yanaonyesha kuwa asasi hazitekelezi jukumu moja linalofanana. Baadhi huzuia migogoro kwa kuhimiza haki, uwajibikaji na mazungumzo kabla ya vurugu; vyombo vya usalama vinaweza kudhibiti vurugu na kurejesha usalama; mahakama na taasisi za ardhi zinapaswa kushughulikia madai ya umiliki na fidia; mashirika ya kijamii na kidini husaidia waathiriwa na kujenga upya mahusiano; vyombo vya habari hutoa taarifa na kufichua ukiukaji; na wapatanishi huwezesha mazungumzo. Tofauti hii ni muhimu kwa sababu kurejesha usalama hakumaanishi kuwa mgogoro wa umiliki umetatuliwa.

Riwaya ya *Kovu Moyoni* inaonyesha kuwa kushindwa kwa asasi mbalimbali kunatokana na sababu zinazohusiana: urasimu na kutowajibika huchelewesha haki; matumizi ya nguvu na vitisho hudhoofisha imani ya wananchi; upendeleo na uchunguzi usiokamilika unaweza kuadhibu wasio na hatia; maslahi ya kisiasa yanaweza kuendeleza uhasama; na hofu inaweza kuzuia viongozi wa dini au vyombo vya habari kutekeleza wajibu wao. Kwa hiyo, tatizo si kutokuwepo kwa asasi pekee bali pia muundo wa mamlaka, uwezo wa taasisi na mazingira yanayozuia uwajibikaji.

Matokeo haya yanahusiana na Njoroge (2013) na Maina (2015) kuhusu nafasi na mipaka ya mifumo ya kisheria, na Nyiri (2014) kuhusu athari za migogoro na mchango wa mashirika na taasisi za kidini. Hata hivyo, uchanganuzi wa kifasihi unaongeza kipengele cha namna asasi hizo zinavyosawiriwa kupitia wahusika na matukio.

Kwa upande wa taaluma ya fasihi, matokeo yanaendeleza hoja ya Gonye na wenzake (2020) na Opondo na wenzake (2025) kuhusu uwezo wa fasihi kuakisi hali ya jamii. Tofauti na tafiti zinazojikita katika uwakilishi wa masuala ya jamii kwa upana, makala hii inaonyesha jinsi usawiri wa asasi unavyoweza kutumika kutathmini wajibu, mipaka na matokeo ya mamlaka katika mzozo wa ardhi.

Nadharia ya Baadaukoloni inaunganisha matukio ya riwaya na historia pana ya umiliki na mamlaka. Urithi wa ukoloni unaonekana katika madai ya ardhi na kutopatikana kwa fidia; mamlaka na unyonyaji vinaonekana katika urasimu, uchochezi na matumizi mabaya ya nguvu; na upinzani na ukombozi vinaonekana katika juhudi za wananchi kutafuta haki, kuanzisha mazungumzo na kukataa mgawanyiko wa kikabila. Hata hivyo, si kila tukio linaweza kuelezwa

kwa urithi wa ukoloni pekee; uwajibikaji wa sasa na maamuzi ya wahusika pia yana uzito.

Kwa sababu hiyo, utatuzi wa kudumu unahitaji mikakati inayoshughulikia chanzo na matokeo ya migogoro: mifumo ya haki inayofikika, uwajibikaji wa viongozi na vyombo vya usalama, ushiriki wa jamii katika maamuzi ya ardhi, taarifa sahihi na mbinu shirikishi za upatanishi. Ushirikiano huo unapaswa kuheshimu haki za waathiriwa na kuepuka kulazimisha maridhiano bila kushughulikia madai ya msingi.

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Hitimisho: Makala hii imebainisha kuwa serikali na vyombo vya usalama vinaweza kurejesha usalama, mahakama zinapaswa kuhakikisha haki, mashirika yasiyo ya serikali na taasisi za kidini zinaweza kusaidia waathiriwa, vyombo vya habari vinaweza kuelimisha na kufichua ukiukaji, wapatanishi wanaweza kuleta pande pamoja, na wananchi wanaweza kujenga mshikamano. Wanasiasa, hata hivyo, wanaweza pia kuchochea migogoro wanapotumia ardhi na tofauti za kijamii kwa manufaa yao.

Makala imeonyesha kuwa udhaifu wa asasi unatokana na urasimu, ukosefu wa uwajibikaji, matumizi mabaya ya mamlaka na maslahi ya kisiasa. Nadharia ya Baadaukoloni imefafanua jinsi urithi wa mifumo ya umiliki na mamlaka unavyoendelea kuathiri jamii, na jinsi wananchi wanavyoweza kuipinga kupitia madai ya haki na mshikamano. Mchango mahususi wa makala katika fasihi ya Kiswahili ni kuonyesha kuwa riwaya inaweza kutathmini si tu chanzo cha mgogoro bali pia mgawanyo wa majukumu, uwezo na mipaka ya asasi katika hatua tofauti za kukabiliana nao.

Mapendekezo: Makala hii inapendekeza kuwa taasisi za serikali zinazohusika na ardhi ziimarishe uwazi, uwajibikaji na utoaji wa maamuzi kwa wakati kuhusu madai ya umiliki na fidia. Vyombo vya usalama vinapaswa kuzingatia haki za binadamu, kufanya uchunguzi huru na kuwawajibisha maafisa wanaotumia vibaya mamlaka. Viongozi wa kisiasa wanapaswa kuepuka kutumia ardhi na utambulisho wa kikabila kuchochea uhasama; badala yake washiriki katika mazungumzo yanayojumuisha jamii zilizoathiriwa.

Vilevile, asasi za kidini, mashirika yasiyo ya serikali, vyombo vya habari na wapatanishi washirikiane katika kutoa msaada kwa waathiriwa, kuelimisha jamii, kufichua ukiukaji wa haki na kuzuia migogoro kujirudia.Tafiti za baadaye zinaweza kuchunguza zaid riwaya nyingine za Kiswahili na kulinganisha namna zinavyowasilisha asasi na mbinu za utatuzi wa mizozo ya ardhi.

MAREJELEO

Childs, P., & Williams, P. (1997). *An introduction to post-colonial theory*. Prentice Hall.

Fanon, F. (1961). *The wretched of the earth*. Grove Press.

Gatimu, S. (2014, August 20). The role of land issues in Kenya's rising insecurity. *ISS Today*. Institute for Security Studies. https://issafrica.org/iss-today/the-role-of-land-issues-in-kenyas-rising-insecurity

Gonye, J., Moyo, T., & Wasosa, W. (2020). Representations of the land reform programme in selected Zimbabwean short stories and Mutasa's *Sekai, Minda Tave Nayo (Sekai, We Now Have the Land)*: A fait accompli? *Global Journal of Sociology and Anthropology*, 9(4), 1–11. https://www.internationalscholarsjournals.com/articles/representations-of-the-land-reform-programme-in-selected-zimbabwean-short-stories-and-mutasas-sekai-minda-tave-nayo-seka.pdf

Habwe, J. (2014). *Kovu moyoni*. Bookmark African Publishers.

Klopp, J. M., & Lumumba, O. (2017). Reform and counter-reform in Kenya's land governance. *Review of African Political Economy*, 44(154), 577–594. https://doi.org/10.1080/03056244.2017.1367919

Maina, M. W. (2015). *Land disputes resolution in Kenya: A comparison of the Environment and Land Court and the Land Disputes Tribunal* [Master's thesis, University of Nairobi]. University of Nairobi Repository. http://hdl.handle.net/11295/95229

Makunike, B. (2014). *Land reform and poverty alleviation in Mashonaland East, Zimbabwe* [Doctoral dissertation, University of the Free State]. University of the Free State Repository. http://hdl.handle.net/11660/1368

Masibo, S. (2015). *Uchanganuzi wa diskosi za ardhi katika kazi za fasihi: Mtazamo wa waandishi wa Kenya kati ya 1980–2012* [Tasnifu ya uzamili isiyochapishwa]. Chuo Kikuu cha Moi.

Mbembe, A. (1992). Provisional notes on the postcolony. *Africa, 62*(1), 3–37. https://doi.org/10.2307/1160062

Mbembe, A. (2001). *On the postcolony*. University of California Press.

Ngũgĩ wa Thiong'o. (1986). *Decolonising the mind: The politics of language in African literature*. Heinemann.

Njeru, M. K. (2018). *Suala la ardhi katika riwaya teule za Kiswahili: Tathmini ya Kovu Moyoni na Kufa Kuzikana*. MA Thesis, Chuka University.

Njeru, M. K., Kobia, J. M., & Musyimi, D. M. (2022a). Motifu ya ukame katika tamthilia za *Janga la Werevu* (Mohamed, 2011) na *Majira ya Utasa* (Arege, 2015). *East African Journal of Swahili Studies, 5*(1), 183–195. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.733

Njeru, M. K., Kobia, J. M., & Musyimi, D. M. (2022b). Usawiri wa motifu za kimazingira katika tamthilia ya Kiswahili: Tathmini ya *Majira ya Utasa* (Arege, 2015). *East African Journal of Swahili Studies, 5*(1), 151–160. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.699

Njogu, K. (2015). *Elections and the possibilities of land in Kenya*. Twaweza Communications Limited.

Njoroge, S. C. (2013). *Limitations of the current land laws in addressing the squatter land problem in Kenya* [Master's thesis, University of Nairobi]. University of Nairobi Repository. https://erepository.uonbi.ac.ke/items/3b63c9d2-bb74-4bae-8291-ed347346c73b

Nyiri, J. K. (2014). *The impacts of ethnic conflict on economic development: The case of post-election violence in Kenya, 2007–2008* [Tasnifu ya uzamili isiyochapishwa]. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Nyukuri, B. K. (1997). *The impacts of past and potential ethnic conflicts on Kenya's stability and development*. USAID Conference Paper.

Omboi, B. M., & Gachaba, L. M. (2014). Factors leading to squatter problem in Rift Valley Province in Kenya. *Journal of Law and Conflict Resolution, 6*(3), 48–55. https://doi.org/10.5897/JLCR11.038

Opondo, S. O., Kanyua, M., & Ntiba, O. (2025). Masuala ibuka yanayowasilishwa katika vikatuni vya Ubongo Kids. *East African Journal of Swahili Studies, 8*(3), 15–32. https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

Said, E. W. (1978). *Orientalism*. Pantheon Books.

Spivak, G. C. (1988). Can the subaltern speak? In C. Nelson & L. Grossberg (Eds.), *Marxism and the interpretation of culture* (pp. 271–313). University of Illinois Press.